


# HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO

Barua pepe:info@nsimbodc.go.tz  
Tovuti:www.nsimbodc.go.tz

S.L.P



MPANDA

Press No: NDC/ICPRU/Press no.12

May 30, 2018

## TAARIFA KWA UMMA/VYOMBO VYA HABARI UUZWAJI WA VIWANJA KATIKA ENEO LA ISINDE HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo **Bw.Mwailwa Smith Pangani** anawatangazia Wananchi wote uuzaji wa viwanja vilivyopo eneo la Isinde katika Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.

Viwanja vitauzwa kwa bei iliyoidhinishwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambapo , Mteja ataruhusiwa kulipa kwa awamu kwa muda wa miezi sita (06).

Viwanja vipo Isinde, karibu na barabara Kuu ya Mpanda-Tabora. Bei ya kiwanja ni Tshs 800 kwa Mita ya Mraba kwa viwanja vya makazi, Tshs 1000 kwa makazi na Biashara na 1500 kwa matumizi ya biashara pekee.

Hivyo, wananchi wote wanaohitaji viwanja wanakaribishwa kufika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Idara ya Ardhi ili kuchagua viwanja wanavyovihitaji.

Aidha kwa wateja waliochagua viwanja awali na hawajalipia viwanja vyao wanatakiwa kuwasiliana na ofisi kabla ya kulpia viwanja hivyo ili kujua kama havijauzwa kwa wateja wengine.

Imetolewa na :

John A.Mganga  
Afisa Habari Mawasiliano na Uhusiano (W)  
Kitengo cha Habari Mawasiliano TEHAMA na Uhusiano,  
Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.